

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA PILI

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO
(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)

01 FEBRUARI, 2016

MKUTANO WA PILI

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO - TAREHE 01 FEBRUARI, 2016

I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Job Ndugai (Spika) alisoma DUA na kulingoza Bunge.

MAKATIBU MEZANI:

1. Charles Mloka
2. Lawrance Makigi
3. Asia Minja

II. HAKI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani:-

- Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa Fedha 2016/2017;
- Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliwasilisha Taarifa ya Kamati juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017;
- Mhe. David Ernest Silinde – Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Mipango aliwasilisha Taarifa ya Upinzani juu ya mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka wa Fedha 2016/2017.

III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

1. OFISI YA WAZIRI MKUU:

Swali Na. 47: Mhe. Mwantumu Dau Haji

Swali la nyongeza: Mhe. Mwantum Dau Haji

2. OFISI YA RAISI (TAMISEMI):

Swali Na. 48: Mhe. Vedasto Edger Ngombale

Swali la nyongeza: Mhe. Vedasto Edger Ngombale

Swali Na. 49: Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba

Swali la nyongeza: Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba

Swali Na. 50: Mhe. Neema William Mgaya

Swali la nyongeza: Mhe. Neema William Mgaya

3. WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na. 51: Mhe. Frank George Mwakasaka liliulizwa na Mhe. David Ernest Silinde

Swali la nyongeza: Mhe. David Ernest Silinde
Mhe. Khatib Haji Kai

4. WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Swali Na. 52: Mhe. Upendo Furaha Peneza

Swali la nyongeza: Mhe. Upendo Furaha Peneza

Swali Na. 53: Mhe. Deo Kasenyenda Sanga

Swali la nyongeza: Mhe. Deo Kasenyenda Sanga
Mhe. Richard Mganga Ndassa
Mhe. Allan Joseph Kiula

5. WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Swali Na. 54: Mhe. Faida Mohammed Bakar

Swali Na. 55: Mhe. Ester Nicholas Matiko
Swali la nyongeza: Mhe. Mch. Peter Simon Mgimwa

6. WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Swali Na. 56: Mhe. Pascal Yohana Haonga

Swali la nyongeza: Mhe. Pascal Yohana Haonga

7. WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

Swali Na. 57: Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa

Swali la nyongeza: Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa

8. WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Swali Na. 58: Mhe. Kabwe Ruyagwa Zitto

Swali la nyongeza: Mhe. Kabwe Ruyagwa Zitto

Swali Na. 59: Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga

Swali la nyongeza: Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga

9. WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Swali Na. 60 : Mhe. Joseph Leonard Haule

Swali la nyongeza: Mhe. Joseph Leonard Haule.

10. WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 61: Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka.

Swali la nyongeza: Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka.

IV. MATANGAZO:

- Wageni wote waliokaa kwenye gallery za Bunge walitambulishwa Bungeni;
- Matokeo ya Michezo Bunge Sports Club na CRDB yalitangazwa;
- Mhe. Mussa Azzan Zungu aliwatangazia wapenzi wa Simba washiriki chakula na timu yao siku ya Alhamisi;
- Mhe. George Mkuchika aliomba Wabunge wa Mkoa wa Mtwara wakutane;
- Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi alitangaza kuwa na kikao na wabunge wanaotoka maeneo ya Wafugaji na Wavuvi.

MWONGOZO WA SPIKA:

1. Mhe. James Kinyasi Millya - alitumia kanuni ya 68(7) kutaka kufahamu kuhusu kauli iliyoripotiwa na ITV jana ambapo alionekana Mkuu wa Wilaya ya Kilindi akiwapa wafugaji siku 14 wawe wameondoka wakati ni kunyume cha Katiba, Ibara ya 15 17 inayotoa uhuru wa kuishi na kwenda popote bila kuvunja sheria.

Kiti kilitoa mwongozo kwa Mbunge kulifuatilia zaidi jambo hilo maana suala hilo halina muda mrefu tangu litokee.

2. Mhe. Tundu Antiphas Lissu – alitumia Ibara ya 63(3) (C) ya Katiba na Kanuni ya 3, 94 (1) na 97(1) kwamba Mpango wa miaka Mitano na wa mwaka Mmoja haijawasilishwa Bungeni.

- Mhe. Emmanuel Mwakasaka alitoa maelezo kuhusiana na Hoja ya Mhe. Tundu Lissu kwa kutumia ibara ya 63(3)(C) ya Katiba na Kanuni ya 3, na 57 na kusema kwamba siyo lazima Bunge lianze na Mpango wa miaka Mitano na pia hakuna Ibara yoyote ya Katiba iliyovunjwa.

3. Mhe. Peter Joseph Serukamba – alizungumzia kuhusu Hoja ya Mhe. Tundu Lissu kuwa Kanuni ya 94 na 3 zinaongelea Mapendekezo ya Mpango, ambapo tarehe 21 Serikali ilitoa Mwelekeo wa Mapendekezo na leo imeleta Errata ili kurekebisha makosa yaliyojitokeza kwa hiyo kilichopo mezani ni Mapendekezo ya Mpango na mwezi Machi Mpango kamili ndiyo utaletwa.

4. Mhe. Zitto Ruyagwa Kabwe –alisema Kanuni ya 94(1) inarejea Katiba na kimantiki Mpango wa miaka Mitano hutangulia ndiyo unafuata Mpango wa mwaka mmoja jambo ambalo halikufanyika. Alishauri Serikali Kutumia Kanuni ya 153 ili kurekebisha kasoro iliyotokea.

5. Mhe. Dkt. Marry Michael Nagu – kuhusiana na Hoja hii alisema Mpango ni mchakato na ni kweli Mpango wa mwaka mmoja ni sehemu ya Mpango wa miaka mitano jambo la msingi ni kusahihisha kasoro ili mjadala uendelee.

7. Mhe. Jenister Joakim Mhagama –alisema Kamati ya Uongozi ambayo Kiongozi wa Upinzani ni sehemu ilikutana tarehe 24/1/2016 na 29/1/2016 na kukubaliana kuwa leo Kanuni ya 94 itenguliwe na ilipanga Ratiba ya Bunge inayofuatwa. Alishauri kiti kisishe miongozo ili Bunge liendelee. Na kiti kilikubali kumpa nafasi atoe hoja ya kutengua Kanuni.

V. HOJA YA KUTENGUA KANUNI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu) alitoa Hoja ya kutengua Kanuni ya 94(1) ili Bunge likae kama Kamati ya Mipango wakati wa Mkutano wa pili badala ya Oktoba – Novemba, 2015. Hoja hii ilikubaliwa na Bunge.

VI. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa pamoja na mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka wa Fedha 2016/2017.

VII. KAMATI YA MIPANGO:

Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia – Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliwasilisha Taarifa ya Kamati juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

VIII. BUNGE KUSITISHWA NA KUREJEA:

Saa 6:45 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10:00. Aidha, saa 11:00 jioni Bunge lilirudia likiongozwa na Mwenyekiti (Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa).

IX. KAMATI YA MIPANGO (Iliendelea...):

Mhe. David Ernest Silinde aliwasilisha Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka wa Fedha, 2016/2017.

Baada ya uwasilishaji huo uchagaji wa jumla ulifuata na wafuatao walichangia:-

1. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile – CCM
2. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba – CCM
3. Mhe. Jesca David Kishoa – CHADEMA
4. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako – CCM

KUHUSU UTARATIBU:

Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe alitumia Kanuni ya 63(3) na kutoa Taarifa kwamba gharama iliyotumika kununua Mabeheba siyo bilioni 238 kama alivyosema Mhe. Jesca Kishoa bali haizidi bilioni 60. Kwa maelezo haya alitaka Kiti kimtaka Mhe. Jesca Kishoa athibitisha maneno yake, ambapo Mwenyekiti alikubali na kumtaka Mhe. Kishoa kuthibitisha jambo hilo.

Mhe. Halima James Mdee katika hili alisema kuwa kwa mujibu wa kanunin 63(4) Waziri Dkt. Mwakyembe ndiye anatakiwa kulithibitisha Bunge kuhusu ukweli wa gharama hizo na siyo Mhe. Jesca Kishoa.

Mhe. Jenister Joakim Mhagama –alisema kwa mujibu wa kanuni 63(4) Waziri Mwakyembe ameshalithibitisha Bunge kwamba fedha zilizotumika siyo zaidi ya bilioni 60 hivyo anayepaswa sasa kuthibitisha ni Mhe. Jesca Kishoa. Kiti kilisisitiza kilishatoa mwongozo kwamba Mhe. Jesca Kishoa ndani ya siku tatu athibitisha maneno aliyoyaongea Bungeni.

5. Mhe. Riziki Said Mngwali – CUF
6. Mhe. Ruth Hiyob Mollel – CHADEMA
7. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa – CCM
8. Mhe. Prosper Joseph Mbeni – CCM
9. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara – CHADEMA

TAARIFA

Mhe. Ally Hassan Omar King alitoa taarifa kwa Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara kwamba Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kupitia kifungu cha 42(1) – (5) ndiyo yenye mamlaka ya kutoa matokea na Tume haijatangaza mshindi kinyume na alivyosema Mhe. Mbunge kwamba Mhe. Maalim Seif Sharif ameshinda jambo ambalo siyo kweli na kumtaka athibitisha . Hata hivyo, Mhe. Mwita Waitara alikataa taarifa hiyo na kushikilia msimamo wake.

Mwenyekiti alitoa maelezo kwamba Serikali kwa wakati mwafaka italitolea maelezo jambo hilo.

10. Mhe. Ester Amos Bulaya – CHADEMA
11. Mhe. Angelina Adam Malembeko – CCM
12. Mhe. Zuber Mohammed Kuchauka – CUF

KUHUSU UTARATIBU:

Mwanasheria Mkuu alitumia kanuni 64(f) (g) na 63 kwamba Mhe. Zuber Mohammed Kuchauka ametumia maneno ya kuudhi aliposema Wazanzibar ni kondoo na kumtaka afute kauli.

Mhe. Tundu Antiphas Lissu alieleza kwamba AG hakutumia Kanuni vizuri alitakiwa atoe wakati Mbunge hajamaliza kusema. Hata hivyo, AG alisisitiza yupo sahihi na Mbunge afute kauli ya kudhalilisha.

Mhe. Zuber Mohammed Kuchauka alipopewa nafasi alisema AG hakuelewa alichomaanisha. Kiti kiliagiza *Hansard* ifuatiliwe kuona alichozungumza.

MWONGOZO WA SPIKA:

Mhe. Edwin Amandus Ngonyani alitumia kanuni 63(1) kwamba Mhe. Zuber Mohammed Kuchauka alisema uongo aliposema watendaji wanaoendesha Reli wana Malori 5000, wakati yeye Ngonyani na Waziri Prof. Mbarawa hawana lori hata moja na hivyo aliomba Mbunge afute au athibitishe kauli hiyo.

Mhe. Tundu Lissu alisema kwa mujibu wa Kanuni ya 63(1) 63(4) yeye ndiye alitakiwa athibitishe kwanza na Mbunge hakutaja mtu yeyote wakati akichangia – Mwenyekiti alieleza *Hansard* itafuatiliwa.

13. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka – CCM

14. Mhe. Sophia Mattayo Simba – CCM

MWONGOZO WA SPIKA

Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangala alitumia kanuni 68(7) akitaka kujua kwa nini Mhe. Tundu Lissu aendelee kupewa nafasi wakati analipotosha Bunge hasa alipotoa maelezo ya kanuni ya 63(3) – 5 aliyotumia AG na Mhe. Edwin Ngonyani wakati walikuwa sahihi yeye akasema wamekosea. Mwenyekiti alisema atalitolea maelezo baadaye.

15. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku – CCM

16. Mhe Joseph Osmund Mbilinyi – CHADEMA

TAARIFA

1. Mhe. Jenister Joakim Mhagama alimtaka Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi afute maneno aliyotumia kusema wanafuata mzuka wa Rais kwamba ni Lugha ya kuudhi na inamdhalilisha Rais. Mhe. Joseph Mbilinyi alikataa kufuta kauli kwa vile hakumaanisha hivyo. Mwenyekiti alisema Hansard iangaliwe na aliendelea kuchangia.

2. Mwanasheria Mkuu alitoa taarifa kwamba Mhe. Joseph Mbilinyi amesema uongo kuhusu Waziri Mkuu kwani hakuzuia Mikutano ya vyama siasa kama alivyosema, Mhe. Joseph Mbilinyi alikataa taarifa hiyo.

17. Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala – CCM

MATANGAZO

- Chaguzi mbalimbali zitafanyika siku ya Ijumaa tarehe 5.2.2016 (TUME, SADC-PF, PAP, IPU na CPA) Fomu za kugombea zinatolewa Ofisini kwa Katibu wa Bunge.

X. BUNGE KURUDIA NA KUAHIRISHWA

Bunge lilirudia na kuahirishwa mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

DODOMA
01 FEBRUARI, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE